

TANGAZO LA SERIKALI Na..... la tarehe....201....

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA 290)**

**SHERIA NDOGO**

Zimetungwa chini ya kifungu Na. 6 na 16(1)

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MINADA NA MIFUGO) ZA**

**HALMASHAURI YA MJI WA NZEGA ZA MWAKA 2016**

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika	1.	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Minada na Mifugo) za Halmashauri ya Mji wa Nzega za Mwaka 2016 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
matumizi	2.	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Nzega.
Tafsiri	3.	<p>Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:</p> <p><b>“Afisa Mwidhiniwa”</b> maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata au Mtumishi aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;</p> <p><b>“Bidhaa”</b> maana yake ni vitu mbalimbali vinavyoweza kupatikana katika duka au eneo la mnada;</p> <p><b>“Dalali”</b> maana yake ni mtu ye yote aliyeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kunadi mifugo mnadani;</p> <p><b>“Halmashauri”</b> maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Nzega;</p> <p><b>“Mkurugenzi”</b> maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa ye yote wa umma aliyeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi;</p> <p><b>“Mfugaji”</b> maana yake ni mtu ye yote au kikundi cha watu au chama kinachojishughulisha na ufugaji wa mifugo;</p> <p><b>“Msimamizi wa Mnada”</b> maana yake ni mtu ye yote au mtaalam wa mifugo</p>

		<p>aliyeteuliwa kusimamia au kuratibu shughuli za mnada;</p> <p><b>“Mifugo”</b> maana yake ni aina zote za wanyama wanaofugwa au wanaoweza kufugwa na binadamu ikiwa ni pamoja na ng’ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe;</p> <p><b>“Ushuru”</b> maana yake ni malipo yanayolipwa na mtu ye yote anayefanya biashara kwenye eneo la mnada;</p> <p><b>“Wakala”</b> maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi aliyeteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.</p>
Wajibu wa kulipa ushuru	4.	<p>(1)Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itatoza ushuru wa minada ya mifugo kwa kila aina ya mifugo inayoingizwa mnadani, ushuru utakaolipwa kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala na kila mnunuzi wa mifugo kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Ushuru huo utalipwa siku ya mnada katika eneo la Halmashauri ambapo mnada huo unafanyika.</p>
Maeneo ya mnada	5.	<p>(1) Halmashauri itatenga maeneo maalum kama minada kwa ajili ya kuuza na kununua mifugo pamoja na bidhaa mbalimbali kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Mifugo yote itapaswa kuuzwa ndani ya mnada kwa muda maalum uliopangwa kwa ajili ya uuzaji na ununujaji wa mifugo kama itakavyopangwa na dalali.</p>
Usimamizi na ukaguzi vitabu vya ushuru	6.	<p>Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa:-</p> <p>(1)Kukagua afya ya mifugo ili kuhakikisha usalama wa mifugo kabla ya kuuzwa;</p> <p>(2)Kumtaka mnunuzi ye yote kuonyesha risiti aliyolipia ushuru.</p>
Makosa na Adhabu	7.	<p>(1) Mtu ye yote ambaye:-</p> <p>(i) atashindwa au kukataa kuonyesha stakabadhi aliyolipia ushuru;</p> <p>(ii) atauza mifugo nje ya mnada;</p> <p>(iii) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;</p> <p>(iv) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru;</p> <p>(v) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilling laki moja (100,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote mbili</p>

	<p>kwa pamoja yaani faini na kifungo.</p> <p>(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa chini ya kifungu cha (1) endapo uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi umesababisha hasara kwa Halmashauri, mtuhumiwa atawajibika kulipa fidia ya hasara iliyotokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi.</p>
--	---

## JEDWALI LA KWANZA

*Limetungwa Chini ya kifungu cha 4*

<i>Aina ya mifugo</i>	<i>Kiwango cha Ushuru</i>
Ng'ombe	5,000.00 kwa siku
Nguruwe	5,000.00 kwa siku
Mbuzi	2,000.00 kwa siku
Kondoo	2,000.00 kwa siku
Bidhaa za vibanda mnadani	1000.00 kwa siku
Ushuru wa Makanyagio	2,000/= kwa siku

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Nzega imebandikwa kwenye Sheria Ndogo kufuatia  
Azimio lilipoitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwai uliofanyika Tarehe  
..... Mwaka.....



.....

**PHILEMON M. MAGESA**  
**MKURUGENZI WA HALMASHAURI**  
**NZEGA MJI**

.....

**WILLIAM W. JOMANGA**  
**MWENYEKITI WA HALMASHAURI**  
**MJI NZEGA**

**Nakubali.....**

**Tarehe .....**

.....

**JOHN POMBE MAGUFULI**  
**RAIS**  
**DODOMA**